

# Ahadi Kubwa Zaidi





**Kijitabu hiki kinasimulia juu ya ahadi kubwa zaidi iliyowahi kufanywa... na kile Mungu alichofanya kutimiza ahadi hiyo.**



## Mungu anakupenda na anatimiza ahadi zake.

Tangu Mungu alipoumba ulimwengu,
aliahidi kuwapenda na kuwatunza
watu wa ulimwengu.

Mara nyingine watu huvunja ahadi zao...
lakini Mungu anapoahidi,
anaitimiza!





## Watu huvunja ahadi zao kwa kufanya vitu vibaya:

- Wanamsahau Mungu.
- Hawamtii Mungu.
- Wanaumizana wenyewe kwa wenyewe.

Mungu anasema kwamba adhabu yetu kwa kufanya mambo haya mabaya ni kwamba hatutaweza kuishi naye.

**Dhambi:** Neno la Biblia la kufikiria, kusema au kufanya mambo ambayo Mungu anatuambia tusifanye.

"Kwa maana wote wamefanya dhambi (wamefanya mambo yasiyofaa) na hawajafika wema kamili wa Mungu."
(Warumi 3:23)





# Mungu alitimiza ahadi yake kwa kumtuma Yesu.

Mungu hakuwahi kuvunja ahadi yake ya kupenda watu. Aliwapenda watu sana hivi kwamba alimtuma Mwanawe Yesu kuishi na watu na kuonyesha upendo wa Mungu.

Yesu alikuja kama mtoto,
na watu wachache tu ndio
walijua yeye ni nani...
**Mwana wa pekee wa Mungu,**
**Mwokozi.**

---

**Mwokozi:** Yesu, ndiye pekee anayeweza kuokoa au kukomboa wengine kutoka kwenye mambo mabaya wanayofikiria, nakusema, nakufanya: dhambi zao.

"Mungu alionyesha upendo wake kwetu: alimtuma Mwanawe wa pekee ulimwenguni."
(1 Yohana 4:9)





Yesu alikua mpaka alikuwa mtu mzima.
Alizungumza kuhusu Mungu, Baba yake,
kwa kila mtu aliyekutana naye.

Yesu aliwaambia watu kuhusu ahadi ya Mungu ya kuwapenda.

Yesu aliwaonyesha
watu jinsi ya kumpenda Mungu
na jinsi ya kupendana.

**Na daima Yeye
alikuwa na wakati
kwa ajili ya watoto!**

**"Yesu aliwaita watoto na kuwaambia marafiki zake, Waacheni watoto wadogo waje kwangu. Msiwazuie." (Luka 18:16)**





Lakini watu wengi hawakumpenda Mungu, kwa hivyo walimwua Yesu.

Yesu aliwaruhusu wamfanyie hivi kwa sababu alikuwa akichukua adhabu ya vitu vyote vibaya ambavyo kila mtu alikuwa amewahi kufanya.

## Yesu alikufa.

Yesu alikufa ili watu wote — watu kama wewe na mimi — waweze kusamehewa kwa kufanya vibaya na waweze kuishi kwa urafiki na Mungu sasa na milele.

**Yesu alikufa kwa ajili yako kwa sababu anakupenda.**

**"Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, Yesu. Yeyote anayemwamini Mwana wa Mungu hatapotea, lakini atakuwa na uzima wa milele." (Yohana 3:16)**

---

**Kusamehe:** Kufanya uchaguzi wa kusamehe au kuondoa adhabu kwa mawazo mabaya, maneno au vitendo.
**Kutumaini:** Kutegemea, au kuwa na hakika ya kitu; kutenda yale unayoamini.





Ahadi ya Mungu haikuisha wakati Yesu alipokufa.
**Sehemu bora ilikuwa bado inakuja.**

Mungu alimfufua Yesu.
Watu wengi walimwona na kuzungumza naye.

## Yesu alifufuka

kuonyesha kuwa yeye ndiye Mungu.
Ana nguvu ya kukusaidia kuacha
kufanya mabaya na kuishi
kwa njia ambayo Mungu
anataka uishi.

**"Nilikuja ili upate kuishi, na kuishi maisha bora jinsi iwezekanavyo."**
**(Yohana 10:10)**





Yesu alirudi ili awe na Mungu.

Kabla hajaondoka, alifanya ahadi zingine...

- Yesu anaahidi kuwa na wewe hata ingawa huwezi kumwona.
- Yesu anaahidi kuwa Rafiki yako wa karibu.
- Yesu anaahidi kukusamehe kwa mambo yote mabaya ambayo umeyafanya.
- Yesu anaahidi kuishi ndani yako
  ...mahali ambapo unapenda na kuumiza
  ...mahali ambapo una furaha na huzuni.
- Yesu anaahidi kwamba ukifa unaweza kuishi naye milele.

Je! Ungependa kumwomba Yesu kuwa pamoja nawe na kuishi ndani yako sasa?

**"Mimi nipo nanyi siku zote."**
**(Mathayo 28:20)**

**"Sitakuacha kamwe."**
**(Waebrania 13:5)**





# Ongea na Mungu...

tumia maneno yako mwenyewe au sala kama hii:

"Mpendwa Mungu, ninaamini Yesu ni Mwanao.
Asante kwamba Yesu alikufa msalabani kwa mambo mabaya niliyofanya.
Tafadhali unisamehe kwa sababu nimefanya mabaya.
Ninaomba kwamba Yesu atakuwa pamoja nami na ataishi ndani yangu daima.
Unisaidie kuwa aina ya mtu unayetaka niwe.
Asante kwa kujibu maombi yangu."

**Je! Ungependa kuomba sala hii sasa hivi?**

Tumaini ahadi ya Mungu kwamba anakupenda na kwamba Yesu atakuwa pamoja nawe.

**Maombi:** Kuzungumza na Mungu iwe kimya kimya au kuongea kwa sauti.

**"Watu wote (wanaume, wanawake, wasichana, wavulana) wanaompokea Yesu na kumwamini wanakuwa watoto wa Mungu."**
**(Yohana 1:12)**





Unapomwomba Mungu akusamehe
na umkaribishe Yesu kuwa pamoja nawe...
**Kwa kweli yuko pamoja na wewe na anaishi ndani yako**
—sasa na kila wakati.

Huwezi kumwona,
na labda hauhisi tofauti yoyote.
Lakini kweli Yesu yuko pamoja nawe!
Aliahidi kwamba atakuwepo...
na Yeye hutimiza ahadi zake kila wakati.

Kila siku, mshukuru Yesu
kwa kuwa yeye yupo pamoja na wewe,
na anakusaidia katika maisha
yako pamoja naye.

---

**Imani** ni kuamini kile hatuwezi kuelewa; kuamini ahadi za Mungu... na Mwana wa Mungu... haijalishi unajisikia vipi.

**"Wewe ni mtoto wa Mungu kwa imani katika Kristo Yesu."**
**(Wagalatia 3:26)**





Hata baada ya kumwomba Yesu kuwa pamoja na wewe,
unaweza kutokuwa na huruma na mtu,
au kusema uongo, au kutotii,
au kufikiria mawazo ya ubinafsi.

Wakati wowote unapofanya jambo ambalo unajua si sawa,
ongea na Mungu.
Kukubaliana na Yeye kwamba yale uliyofikiria,
kusema au kufanya, sio yale Yeye anataka ufanye.

Mpe Mungu shukurani
kwa kukusamehe.

**Kukiri:** Kusema ukweli juu ya Mungu ni nani; kumwambia Mungu unakubaliana naye kwamba kile ulichofanya kilikuwa kibaya.

**"Ikiwa tunakiri dhambi zetu, Mungu ni mwaminifu na wa haki hata kutusamehe na kutusafisha kutokana na ubaya ambao tulifanya."**
**(1 Yohana 1:9)**

**Mungu ametoa ahadi zingine nyingi za ajabu.**
Ameahidi kukusaidia kukua katika maisha yako mpya na Yesu.





Unaweza kuanza kujua ahadi za Mungu...
...kwa kusoma mistari ya Biblia kwenye kitabu hiki.
...kwa kwenda mahali ambapo watu hufundisha kuhusu Yesu.
...kwa kuzungumza naye kila siku.

Unaweza kuambia familia yako na marafiki zako mambo ambayo umejifunza kuhusu Yesu.
Unaweza kuwasomea kitabu hiki na uwasaidie kumwomba Mungu awasamehe.
Kwa msaada wako wanaweza kumwomba Yesu kuwa pamoja nao na kuishi ndani yao.

Na kila wakati,
**amini ahadi za Mungu...**
**Yeye hufanya kile Yeye anachosema.**

**Ahadi yangu...**

**Leo, nilipoomba, Mungu alinisamehe kwa mambo mabaya ambayo nimefikiria, kusema, na kufanya.**
**Kwa sasa Yesu yuko pamoja nami na anaishi ndani yangu.**
**Nataka kuwa mtu wa Mungu jinsi ambavyo anataka niwe.**
**Nataka kukua katika kumpenda Mungu na watu wengine.**

Jina langu: ______________________

Tarehe: ______________________



Imeandikwa na Vernie Schorr

Swahili

Imetafsiriwa kwa Kiswahili na Stacy Collins
Imehaririwa na Tegemea Mbise
©1990 The JESUS Film Project
Imechapishwa na Foursquare Missions Press kwa ruhusa.

Mistari ya Biblia katika kitabu hiki imeandikwa kwa urahisi wa kuelewa.

Picha kwenye kijitabu hiki kinachotumiwa na ruhusa ya The JESUS Film Project na kuchukuliwa kutoka “JESUS,” filamu ya masaa 2 kuhusu maisha ya Kristo. Kwa habari zaidi kuhusu filamu ya “The Story of Jesus for Children” au vifaa vingine, wasiliana na: The Story of Jesus for Children, 910 Calle Negocio, Ste. 160, San Clemente, CA 92673, USA, 1-800-432-1997, www.jesusforchildren.org